yao wayafanyao kama haya.
3 Wathani, ee mtu, uwahukumuye wayafa-
nyayo, ukayafanya wewe, kama utaokoka
4 katika hukumu ya Muungu? Ao wingi wa
wema wake, na upole, na uvumilivu, umeu-
tharau, usipojua kama wema wa Muungu
5 wakuongoa utubu? Illa katika ugumu wa-
ko na moyo usiotubu wajiwekea hasira kwa
siku ya hasira na kufunuka hukumu ya ha-
6 ki ya Muungu atakayemlipa killa mtu, kwa
7 matendo yake. Kwao watafutao katika
kustahimili, wakitenda vema, sifa na heshi-
8 ma na kutoa kuharibika, uzima wa milele;
kwao wasiotulia, wasioyafuata ya kweli,
9 wayafuatayo ya thulumu, hasira na ghathabu.
Mateso na shidda kwa killa roho ya mtu
10 mtenda uovu, Myahudi kwanza, tena Myo-
nani. Sifa na heshima na amani kwa killa
11 atendaye mema, Myahudi kwanza, tena
Myonani. Kwani hapana upendeleo wa mtu
12 kwa Muungu. Waliokosa pasipo torati, wa-
tapotea pasipo torati, waliokosa wakiwa na
13 torati watahukumiwa kwa torati. Kwani sio
wasikiao torati walio na haki mbele ya Muu-



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

ngu, illa watendao torati watakuwa na haki.
14 Kwani mataifa wasio na torati wakifa-
nya kwa asili yaliyo katika torati, hawa wa-
sio na torati wamekuwa torati yao wenyewe,
15 waithihirisha kazi ya torati imeandikwa mi-
oyoni mwao, thamiri ikiwashuhudia, mawa-
zo yao yakishtakiana ao yakiachiliana.
16 Siku ile Muungu atakapohukumu siri za
waana Adamu kwa anjili yangu, *iliyo* kwa
Isa Masiya.
17 Ukiwa umekwitwa Myahudi, ukatege-
18 mea torati, ukajisifu kwa Muungu, ukamjua
apendalo, ukayapambanua yaliyo bora, uki-
19 elimishwa na torati, ukijithania mwenyewe
kiongozi cha vipofu, mwanga wao walio gi-
20 zani, mkufunzi wao wasio na akili, mwalimu
wao watoto, ukiwa na namna ya hekima na
21 kweli katika torati. Umfundishaye mwi-
ngine hujifundishi mwenyewe? Uhubiriye
22 wasiibe, umekwiba? Unenaye wasizini, u-
mezini? Uchukiaye sanamu, umeyatwaa
23 yaliyo wakf? Ujisifuye kwa torati, kwa
kuikosa torati umemtharaulisha Muungu?
24 Kwani jina la Muungu limenenewa unajisi



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

katika mataifa kwa ajili yenu, kama yalivyo-
25 andikwa. Tohara hufaa ukiishika torati,
ukiwa mvunja torati, tohara yako umekuwa
26 lisilo tohara. Pasipo tohara hukumu za to-
rati zikishikwa, pasipo tohara isihesabiwe
27 kuwa tohara? Pasipo tohara, iliyo kwa asili,
torati ikishikwa, itakuhukumia wewe uliye
28 na andiko na torati illa umeivunja torati.
Kwani siye Myahudi aliye kwa wazi, wala si
29 tohara iliyo kwa wazi katika mwili. Ndiye
Myahudi aliye kwa ndani, na tohara ya mo-
yo katika roho wala si katika andiko, yenyi
sifa si kwa watu, illa kwa Muungu.
III. Bassi Myahudi amezidije, na tohara ya-
2 faa nini? Sana kwa pande zote. Kwanza
kwani wameamriwa ayanenayo Muungu.
3 Nini tena, wangine wasipoamini? Kutoa ku-
amini kwao kutabatili imani ya Muungu?
4 Hasha. Muungu awe na kweli na killa mtu
'mwongo, kama ilivyoandikwa, Illi uwe na
haki katika maneno yako, ukashinde uhu-
kumiwapo.
5 Kama thulumu yetu imefanya imara haki
ya Muungu, tusemeje? Muungu hana haki



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

atuletaye hasira? (nanena kwa mwana ada-
6 mu) Hasha. Ginsi gani Muungu angehuku-
7 mu ulimwengu? Kwani kweli ya Muungu
ikizidi kwa uwongo wangu, kwa kusifiwa Ye-
8 ye, hatta hivi kama akosaye nahukumiwa,
wala si, kama tumenenewa unajisi, na kama
watu husema tumenena, Tuyafanye mabaya,
mema yakaje. Wahukumiwao kwa haki.
9 Nini tena? Tumetangulia? Siyo kabisa.
Kwani tumewastaki na Wayahudi na Wa-
10 yonani wote wako katika thambi. Kama
yalivyoandikwa, Hapana mwenyi haki hatta
11 mmoja, hapana ajuaye, hapana amtakaye
12 Muungu. Wamekosa wote, wameoza pa-
moja. Hapana atendaye mema hatta mmo-
13 ja. Koo lao li kaburi wazi, kwa ulimi wao
hufanya hila. Sumu ya majoka chini ya
14 midomo yao. Kinwa chao kimejaa laana
15 na uchungu. Miguu yao mipesi kumwaga
16 damu. Mathara na ubaya njiani mwao, wa-
17 la njia ya amani hawakuijua. Hapana hofu
18 ya Muungu machoni pao.
19 Twajua kama inenayo torati yanena kwao
walio chini ya torati, killa kinwa kizibwe,



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

ulimwengu wote ustakiwe mbele ya Muu-
20 ngu. Kwa sababu katika matendo ya sheria
hapana kufanyiziwa haki mtu wo wote mbe-
le yake. Kwani kwa sheria, hujulikana
makosa.
21 Sasa pasipo torati haki ya Muungu ume-
onekana, iliyoshuhudiwa na torati na nabii.
22 Haki ya Muungu kwa imani ya Isa Masiya
katika wote na juu ya wote waaminio; ha-
23 pana tofauti, wote wamekosa, wamepungu-
24 ka utukufu wa Muungu, wakafanyika kuwa
na haki burre kwa neema yake kwa ukombo-
25 zi ulio wa Masiya Isa, aliyemtoa Muungu
upatanisho kwa imani katika damu yake.
Kuonyesha haki yake katika kuziachilia
thambi zilizotangulia akivumilia Muungu.
26 Kuonyesha haki yake wakati huu, akiwa
mwenyi haki na mfanyiza haki kwake *aliye*
wa imani wa Isa.
27 Wapi tena kusifu? Kumeondolewa. Kwa
sheria gani? Ya matendo? Siyo, illa kwa
28 sheria ya imani, kwani twahesabu mtu ku-
fanyiziwa haki pasipo matendo ya torati.
29 Ni Muungu wa Wayahudi tu? Siye tena



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

30 wa mataifa? Na'am, wa mataifa tena, Muu-
ngu akiwa mmoja afanyaye haki kwao wa-
liotahiriwa katika imani na kwao wasiotahi-
31 riwa kwa imani. Sheria hatukuitangua
kwa imani? Hasha, sheria tumeifanya imara.
IV. Tusemeje tena Ibrahimu baba wetu ame-
2 ona nini katika mwili? Kwani Ibrahimu
akipata kuwa na haki kwa matendo, anayo
3 ajisifie, illa si kwa Muungu. Kwani nini ma-
andiko yasema, Ibrahimu akamwamini Mu-
4 ungu ikahesibika kwake kuwa haki. Ate-
ndaye ijara yake haihesabiki kuwa neema,
5 illa kuwa deni, asiyetenda aliyemwamini
awafanyiaye haki wanajisi, imani yake ya-
6 mhesabika kuwa haki. Kama anavyonena
na Daud heri yake mtu, Muungu aliyemhesa-
7 bia haki pasipo matendo, Heri walioondole-
8 wa makosa, na thambi zao zimestirika. Heri
ndiye mtu asiyemhesabia Bwana thambi.
9 Heri tena hii kwao waliotahiriwa ao kwao
tena wasiotahiriwa? Twasema kama imani
10 imemhesabikia Ibrahimu kuwa haki. Ime-
hesabikaje, akiwa ametahiriwa ao asipota-
hiriwa? Si alipokwisha kutahiriwa illa asi-



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is